Jamii Ya Kimisheni

(Missionary Society)

Na J D Logan

Huu ulikuwa ni upotofu wa kwanza kuonekana miongoni mwa makanisa ya Kristo. Ilisababisha madhara makubwa ya kuondoka katika kielelezo cha maandiko, inaondoa jukumu la kanisa katika kueneza Injili.

Ukweli Wa Kihistoria

Jamii ya Misheni ya Kikristo ya Amerika walikuwa na mizizi yao katika kile tunachosema kwamba ni "Vuguvugu la urejesho". Mapema 1800 vuguvugu la kidini ijulikanayo "muamsho mkuu" iliyoanza katika sehemu ya magharibi mwa Amerika na mara ikasambaa katika sehemu zingine za nchi. Watu wakaanza kusisitiza waumini katika Kristo wanaapaswa kuacha mafundisho ya madhehebu, majina, na mifumo ya ibada, na kutoa wito kwa "ndivyo yanenavyo maandiko" katika mafundisho yote, imani na matendo katika ibada.

Kuliinuka baadhi ya watu wachache waliokuwa wahubiri mashuhuri na waalimu wa neno la Mungu, miongoni mwao ni John "Raccoon" Smith, Barton Stone, Thomas na Alexander Campbell, miongoni wa wengine. Mara wale wwaliofuata mifumo hii waliunda makusanyiko tofauti na madhehebu yalioko jirani nao naa wakaanza kuweka vipengele hivi katika vitendo. Walijiita wenyewe kama "Makanisa ya Wakristo" na "Wanafunzi wa Kristo". Makusanyiko haya yakakua ghafla na ushirika pia ukakua katika kiwango cha hali ya juu sana.

Kanisa lilivyokuwa linakuwa, baadhi ya wahubiri na waalimu walihisi kwamba kanisa lilihitaaji msaada katika kuendeleza "agizo kuu". Hawakuridhika na muongozo wa maandiko wa kanisa katikaa urahisi wake na wakaanza kutengeneza vitu ambavyo si vya kimaandiko na jamii wafanye kazi hii muhimu.

Oktoba 23, 1849, katika Cincinnati, Ohio, kulikuwa na mkutano ulioandaliwa na wakuu wa kanisa kwa ajili ya kusudi la kueleza mwendelezo wa kazi na kanisa kwa ujumla. Wakatika wa mkutano huu, "Jamii ya Kikristo ya Amerika" liliundwa. Watu maarufu katika mkutano huu alikuwa ni W. K. Pendleton, mkwe wa Alexander Campbell.

Kwa maneno ya William J. Wright wa Cincinnati, Ohio, (1910 Taarifa ya Mkutano Mkuu) "vuguvugu letu halina halina mpangilio wa misheni". "…ushindi wa Amerika na nchi zilizoko mbele haikuwezekana isipokuwa wezi na majambazi walipigwa katika jeshi." Alikuwa anawaongelea wahubiri na wafanya kazi wa "vuguvugu la kidini", (Smith, Campbell, Stone, n.k) pamoja na wafanyakazi wakuu walioendeleza kazi hii ya kurejesha Ukristo wa kwanza katika usafi wake.

Mijadala katika Kutetea "Jamii"

1. Kwamba juhudi hii ya urejesho uli, na lina mafanikio lilionekana wazi kwamba vuguvugu lilikuwa linakuwa kwa haraka ulimwenguni. Kwa nini ilikuwa ni muhimu kuongeza wazi mafanikio ya ishara tofauti na ukiachilia mbali kanisa? Kwamba ilikuwa wazi kwa wachochezi kwamba liwe shirika tofauti na kanisa inaonyeshwa wazi kwa taarifa ifuatayo katika sherehe ya 100 ya Jamii ya Misioni. "Ilikuwa muhimu kuonyesha jinsi gani vifaa vya mwanadamu vimefanya kazi kiasi gani katika kanisa vilikuwa vinashaurika au kuruhusiwa kama imani, ibada, na huduma zilipaswa kuwa safi. Tunawezaje kulirejesha kanisa la karne ya kwanza, na mwongozo na mifumo ambayo haijaelezwa katika Agano Jipya?"

   Mwitikio zaidi ya waliounga mkono Jamii hiyo ni kwamba ilikuwa geni katika mafundisho ya Agano Jipya ni yafuatayo: "Wasiotaka mabadiliko na wahalisia waliita jamii wavumbuzi na kosa. Baba waliamua kwamba kurejesha katika ukamilifu kanisa la mitume ilikuwa ni sahihi au Mkristo.

   Inastaajabisha!! Hii haihitaji jibu kwa upande wangu!!
2. Mvutaano mwingine wa waanzilishi wa "jamii" hii ilikuwa…" Kushikilia mawazo yanayofanana, kuwa na ubunifu unaofanana au umahiri, kushiriki imani inayofanana, au hata kushikilia imani ya dini hakuanzishi undugu…" Ilikuwa muhimu, kwa maneno yao, kuundanda shirika lisilo la kimaandiko ili kuleta udugu wa kweli. Ni ufanisi ulioje wa kupendekezaa kwamba mitume wa Bwana na makusanyiko walioanzisha waalishindwa kutimiza wajibu waliopewa na Bwana wakianzisha "jamii" iliyotengenezwa na mwanadamu.

   Jibu

   Kwa maneno ya Paulo, "*Basi ndugu zangu nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.*" (1 Kor. 1:10). Huu ulikuwa mpango wa Mungu kupata undugu!!

   Inaokana kwamba wale wanaoshikilia "jamii" hii wanajikuta wako kinyume na mpango wa Mungu!!

   "Undugu" unaanzishwaje? Msikilize Paulo tena. Kwa watakatifu na ndugu waaminifu walio katika Kristo katika Kolosai…" (Kol.1:2). "*Wasalimuni ndugu walioko Laodikia na Nimfa, na kanisa lililoko katika nyumba yake.*" (Kol. 4:15). Hapa, Paulo aliamini kwamba kanisa lilianzisha "undugu". Kulingana na wengine, kwa miaka 1849, kanisa la Kristo limeshindwa kutimiza kazi iliyopewa na Mungu, kulingana na mtindo ulioanzishwa na mitume (kanisa la sehemu moja lililo na wazee) ikifanya muhimu kwa watu kuanzisha "jamii" kufanya kazi hii.

   Katika mlolongo huu wa vitu, makusanyiko yalipaswa kupangilia vyanzo vyao kutoka katika vitengo vya nje, ambazo kwa zamu zifanye kazi iliyotolewa kwa kila kusanyiko la

mahali fulani na wazee wake. Hii ilifanywa mapema katika jaribio la ushirika na mgawanyiko ulifanywa katika kanisa.

Bwana Pendleton alibisha kwamba jukumu la kanisa lilikuwa ni kuhubiri injili kwa ulimwengu wote; lakini hakuaninisha mfumo wa kufanya hilo liwezekane. Alifikiria kwamba mfumo wowote ambao kanisa litachagua kufanya itakubalika.

Bwwana Pendleton alifikiria zaidi kwamba kwa vile hakuna pingamizi iliyoonyeshwa (katika maandiko) kwa jamii, basi sio mfumo wa kimaandiko.

Jibu

Hii ni aina moja wapo ya fikira inayotumiwa kudhihirisha nyongeza yote katika kazi na ibada ya kanisa. Ikiwa kitu chochote kinakubaliwa kwa sababu tu haijakataliwa katika maandiko, hakuna ukomo katika uvumbuzi tunaoweza kuanzisha. Kwaya, muziki, maigizo (Nafahamu baadhi ya haya)**,** ubatizo wa watoto wachanga, vyombo vya muziki (Vilianzishwa na watu hao muda mfupi) kufukiza uvumba, mishumaa, "maji matakatifu" …orodha haina mwisho. Mwishoni, kinachoitwa "kanisa la Kristo" hawawezi kuwa na mfanano wa kanisa tunalolisoma katika Agano Jipya.

Kwa ufupi, hili lisingekuwa kanisa lililorejeshwa, kwa namna yo yote ile, isipokuwa ni dhehebu tu kama madhehebu mengine!!

Ben Franklin, kwenye marudio ya Mkristo wa Marekani, mnamo Mai 7, 1867, aliandika, "Mazingira ya kwamba hawakuwa na jamii ya kimisheni wakati wa kwanza wa kanisa, yake binafsi, haidhihirishi kwamba tunapaswa kuwa nao. Lakini ukweli kwamba Bwana alichagua makusanyiko, na viongozi wao, na akaifanya kuwa kazi yao ya kuongoa ulimwengu kwa ukweli wa nyongeza kwamba tuna mifano yao ya kuwatuma wahubiri, kwa mazingira hayo, kwamba hawakuwa na jamii ya kimisheni, lakini makanisa yanathibitisha kwamba ni makosa kwa watu wachache kuunda jamii ya kimisheni, tofauti na makanisa ya sehemu, kama mbadala wa kufanya kazi ambayo Bwana ametoa kwa makanisa…Swali rahisi ni, kama tutaheshimu makanisa kuzifanyia na kuzifanya ziwe na nguvu kama jamii iliyoteuliwa na Bwana, katika kuongoa ulimwengu, au kuwatangazia kwamba hawafai kufanya kazi ambayo Bwana amewapa, na kubadilisha uumbaji wa mikono yetu wenyewe, kufanya kazi ya makanisa iliyotolewa na Bwana."

David Lipscomb aliandika katika Msimamizi wa Injili, Feb 7, 1867, "Kufanya kazi kupitia kitengo ambacho wanadamu ndio waamzi katika kanisa la Mungu, kwa upande wetu, kumuinua mwanadamu kana kwamba ni mkuu kuliko hekima na uwezo wa Bwana."

Jacob Creath aliandika katika Msimazi wa Ijili, Jan 6, 1866, "…Ukristo wa kigeni ulitangazwa na watu fulani, na siyo jamii au mawakili, kama ilivyo injili ya kisasa…Kanisa la Yerusalemu lilitangaza injili, au washirika wake kila mmoja, baada ya ufufuo wa Kristo, kabla ya kanisa nyingine kuweza kulisaidia kupitia Yudea, Samaria, Phenisia, Cypras, Antiokia…katika karne ya kwanza ya wakati wa Ukristo (Mdo. 1, 2 na 11) Kama kanisa mama na mfumo wake ilivyotangaza injili, ndivyo yalivyofanya makanisa kila mmoja (siyo katika jamii), kama Antiokia huko Ashuru (Mdo. 13), na

Thesalonike walikuwa wazuri katika injili ndani ya Makedonia na Akaya (1 Thes. 1:8). Kanisa lolote sasa linaweza kufanya vivyo hivyo kama makanisa ya kwanza yalivyo fanya; kila mshirika na afanye kile anachoweza kufanya kuhubiri injili. Kama kanisa au mtu hawezi kufanya kitu ili atangaze injili, hakuna kinacho hitajika kwa mtu huyo…"

Tunaweza kuchukua mifano ya makanisa la karne ya kwanza katika mioyo yetu, pamoja na hawa wafanya kazi waliofanya kazi kwa bidii karne ya kumi na tisa, kama mifano yetu na kukataa yote ya "jamii" kama hazifai.

J. D. Logan